

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
WAKALA WA UFUNDI NA UMEME (TEMESA)



TANGAZO LA KAZI

KAZI YA MUDA

Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria Na 30 ya mwaka 1997. Majukumu yake makubwa ni kutoa huduma za matengenezo ya magari na mitambo, huduma za Umeme ikiwa ni pamoja na kufanya matengenezo ya taa za barabarani, kufanya matengenezo ya majokofu, viyoyozi na kufanya matengenezo ya mifumo ya TEHAMA na vifaa vya elektroniki, kutoa huduma za vivuko na huduma za ushauri.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wakala yanatekelezwa anatangaza nafasi za kazi za muda kwa ajili ya Vituo vya TEMESA Pwani, Mwanza, na Magogoni Feri kama ifuatavyo:

NAHODHA WA KIVUKO - NAFASI 30

Sifa za mwombaji:

Mwombaji anatakiwa kuwa na elimu ya kidato cha nne au kidato cha sita pamoja na mojawapo ya sifa zifuatazo;

- i. Awe na "Class 4 Certificate of Competence" (COC)

Au;

- ii. Awe na "Class 4 Certificate of Competence" (COC) pamoja na "Master Near Coast"

Au;

- iii. Awe na Class 3 Certificate of Competence (COC)

NB: Waombaji wenye Shahada au Stashahada katika fani ya "Navigation", "Mechanical Engineering" na "Marine Engineering" watafikiriwa pia.

MAJUKUMU

- i. Kuendesha na kuongoza Kivuko;
- ii. Kutoa maelekezo ya kufunga na kufungua kamba za Kivuko;
- iii. Kusimamia usalama wa abiria na mizigo ndani ya Kivuko;
- iv. Kusimamia upangaji wa abiria na mizigo kwenye Kivuko;
- v. Kuhakikisha kwamba injini ya Kivuko zipo katika hali nzuri ya kufanya kazi;
- vi. Kuangalia mafuta na vyombo vingine vya kufanyia kazi;
- vii. Kutunza daftari la safari za Kivuko;
- viii. Kutunza nyaraka muhimu za Kivuko;
- ix. Kusimamia nidhamu na utendaji wa watumishi walio chini yake;
- x. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania.
- ii. Barua za maombi ziambatishwe na nakala za vyeti husika pamoja na nakala ya cheti cha kuzaliwa, picha mbili ndogo (passport size) za mwombaji na taarifa binafsi (curriculum vitae) ya mwombaji.
- iii. Waombaji watakaokuwa na sifa zinazohitajika ndio watakaoitwa kwenye usaili.

Barua za maombi zitumwe kwa:

Mtendaji Mkuu,
Wakala wa Ufundi na Umeme,
S. L. P. 1075,
DODOMA.

AU KWA;

Meneja Mkoa,
Wakala wa Ufundi na Umeme,
S. L. P. 30150,
KIBAHA - PWANI.

AU KWA;

Meneja Mkoa,
Wakala wa Ufundi na Umeme,
S.L.P. 691,
MWANZA.

AU KWA;

Mkuu Wa Kivuko,
Kivuko Cha Magogoni,
Wakala wa Ufundi na Umeme,
S.L.P. 9691,
DAR ES SALAAM.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 21 Januari, 2021.